

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu +255 22 211 3165  
Nukushi: +255 22 212 4576  
Barua pepe: cl@ardhi.go.tz  
Unapojibu tafadhali taja:



1 MTA A WA ARDHI,  
S.L.P. 9132,  
11477 DAR ES SALAAM,

Kumb. Na. LD/388380/24  
Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke  
S. L. P 46343,  
DAR ES SALAAM.

06/02/2023

**YAH: KUMILIKISHA KIWANJA NA P.16179 ENEO LA VIWANDA MBAGALA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MANISPAA YA TEMEKE KWA AJILI YA  
UWEKEZAJI.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.


2. Tunakiri kupokea barua yenye Kumb. Na. TMC/LD/MBG/33921/LRC ya tarehe 15/12/2022 iliyojibu barua yetu LD/388380/16 ya tarehe 12/12/2022.

3. Kwa mujibu wa barua hiyo inaelezwa kiwanja tajwa hapo juu kimetokana na kuunganishwa kwa viwanja Na. 831, 832 na 833 Kitalu "M" Mbagala na kisha vikapimwa upya ili kupata kiwanja kinachokidhi mahitaji ya uwekezaji unaolengwa. Hata hivyo baada ya kupitia viambatisho vilivyowasilishwa tunaona kuna ufafanuzi haujatolewa:-

- (i) Viwanja Na. 831, 832 na 833 Kitalu "M" Mbagala kabla ya kuunganishwa na kupimwa upya vilikuwa na jumla ya ukubwa wa mita za Mraba 1939. Hata hivyo ukubwa wa kiwanja Na.P16179 Mbagala mita za Mraba 3333. Hivyo, tunaomba kupata taarifa inayo oneshwa eneo lililoongezeka baada ya upimaji limetokana na eneo gani.
- (ii) Kwa kuwa viwanja Na. 831 na 832 Kitalu "M" Mbagala vinahusiana na mirathi, ni muhimu kuhakikisha warithi wanawasilisha nyaraka ya kisheria ya kuridhia makubaliano yaliyofikiwa baina ya msimamizi wa mirathi na Mwekezaji.
- (iii) Kwa kuwa kiwanja (P.16179) kinachokusudiwa kumilikishwa kimetokana na mauziano kutoka kwa wamiliki wa awali kwenda kwa Mwekezaji, tuwasilishiwe uthibitisho wa kulipwa kwa kodi ya ongezeko la Mtaji (Capital Gains Tax).

4. Aidha tunapenda kukumbushia kuwa lengo la uhakiki unaofanyika ni kuhakikisha tunatoa miliki zilizo salama kwa wawekezaji ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza baada ya hatua za umilikishaji kukamilika. Hivyo tunategemea mapungufu haya yatarekebishwa mapema ili kutuwezesha kuendelea na hatua ya umilikishaji.

Tunategemea ushirikiano wako.

  
Bishanga, T.H

**K.n.y: KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI  
MKOA WA DAR ES SALAAM**

Nakala:           Mkurugenzi Mtendaji  
                  Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)  
                  S. L. P 938,  
                  **DAR ES SALAAM**           (Kwa taarifa)

                  Mkurugenzi Mtendaji  
                  Argentina Plas Co Ltd  
                  S. L. P 20386,  
                  **DAR ES SALAAM**           (Kwa taarifa na ufuatillaji)